**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

**Mtaa wa Mahakama,**
**S. L. P. 1419,**
**53103 MBEYA.**
**Simu: (025) 252503566**
**Nukushi: (025) 252502958**
**Barua pepe:**
**rbcmbeya@pccb.go.tz**
**Wavuti: http://www.pccb.go.tz**

**MBEYA – JULAI, 2020**

**TAARIFA KWA UMMA**

**TAKUKURU MBEYA YAZIDI KUWABANA WADAIWA SUGU NA KUOKOA ZAIDI YA SHILINGI MILIONI MIA NNE**

Katika kipindi cha mwezi April hadi Juni 2020 TAKUKURU mkoa wa Mbeya iliendelea kuwabana wadaiwa sugu wanaodaiwa na vyama vya ushirika (AMCOS), vyama vya kuweka na kukopa, Halmashauri na taasisi mbalimbali zinazohusika na ukusanyaji wa kodi ya mapato serikalini na kufanikiwa kuokoa kiasi cha Tshs 406,485,000.28.

TAKUKURU Mbeya ilifanya ufuatiliaji wa fedha hizo katika wilaya zote za mkoa wa Mbeya na kufanikiwa kurejesha fedha kama ifuatavyo: -

- kiasi cha shilingi 205,379,805.00 kimeokolewa kutoka kwa watumishi ambao walipewa jukumu la kukusanya mapato kupitia mashine za kielectroniki (POS) na hawakuwasilisha mapato hayo waliokusanya kwa wakati katika Halmashauri zao.

- kiasi cha shilingi 10,858,395.28 kimeokolewa kutoka kwa Diwani aliyemaliza muda wake ambapo fedha hii ilikabidhiwa kwake kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule ya sekondari Amos Makala iliyoko katika wilaya ya Chunya na yeye kuichukuwa kama mali yake binafsi.

- kiasi cha shilingi 177,175,330.00 kimeokolewa kutoka katika vyama vya ushirika ambapo ni fedha zilifujwa na viongozi wa vyama na mikopo ambayo ilikuwa haijarejeshwa na wanachama waliokopa.

- kiasi cha shilingi 6,880,000 ni fedha ambazo ziliokolewa kutoka kwa vikundi mbalimbali vilivyokuwa vimekopeshwa na Halmashauri kutoka katika fungu la asilimia 10 la mapato ya ndani, kwani vikundi hivi vinapokopeshwa hutakiwa kurudisha fedha hiyo kwa wakati kama ambavyo wanakuwa wamepangiwa.

- kiasi cha shilingi 6,191,470 ni fedha zilizookolewa kutoka katika sekta za ujenzi, mabaraza ya kata, ardhi na binafsi. Ambapo fedha hizo ni tozo mbalimbali

ambazo zilikuwa haziwasilishwa mamlaka husika ikiwemo mamlaka ya mapato Tanzania.

**UZUIAJI RUSHWA**

TAKUKURU mkoa wa Mbeya kwa kipindi cha April hadi juni 2020 ilifanya chambuzi za mifumo 6, vikao vya wadau 5 na ulifuatilia taarifa 3 za utekelezaji wa maamuzi baada ya vikao vya wadau.

Moja ya uchambuzi wa mfumo uliofanywa na ofisi yetu ulihusu upangaji wa vibanda vinavyozunguka katika kituo kikuu cha mabasi ya mikoani na baada ya kufanya uchambuzi huo, tuliweza kubaini kuwa vibanda vingi vilivyopo katika kituo cha mabasi ya mikoani vilipangishwa kwa wafanyabiashara ambao nao walivipangisha kwa watu wengine kwa kodi kubwa tofauti na inayotozwa na Halmashauri.

Pia tulibaini kuwa baadhi ya wafanyabiashara walipangishwa na halmashauri ya jiji wamefanya mabadiliko kwenye baadhi ya vibanda walivyopangishwa kwa kuongeza vyumba vingine bila ya idhini ya halmashauri ya jiji kinyume na mkataba wa upangaji kati halmashauri ya jiji na mpangaji.

TAKUKURU baada ya kubaini hayo ilikaa na wadau wa stendi kuu ambao ni uongozi wa halmashauri ya jiji, uongozi wa wafanyabiashara na kujadili yaliyobainika na kutoa mapendekezo.

Moja ya mapaendekezo ilikuwa halmashauri ya jiji ifanye uhakiki wa wafanyabiashara wanaofanya biashara katika vibanda vya halmashauri, pia Halmashauri ya jiji la Mbeya ilishauriwa kutengeneza mikataba upya kwa wale wafanyabishara waliobainika wanalipa kodi mara mbili yaani kwa watu waliowapangishia na halmashauri ya jiji.

Halmashauri ya jiji la Mbeya baada ya kufanya uhakiki wa awali katika vibanda 93 katika kituo kikuu cha mabasi iligundua kuna wafanyabiashara wapatao 33 walipangishwa na watu binafsi na vibanda 12 vilifanyiwa upanuzi bila idhini ya halmashauri ya jiji. Hivyo kutokana uchambuzi huu wafanyabiashara wapatao 33 wanatarajiwa kupatiwa mikataba ya Halmashauri ndani ya mwezi julai 2020 hivyo kupunguziwa mzigo wa kulipa kodi mara mbili.

TAKUKURU iliendelea kufanya ufuatiliaji wa fedha za maendeleo, kwa kufanya ukaguzi kwenye miradi ya ujenzi, katika sekta ya elimu ambapo ilikagua miradi ya ujenzi wa madarasa, vyoo na ofisi za walimu vyenye thamani ya Tsh **22,000,000/=** na kushauri hatua mbalimbali ikiwemo kuhakikisha vifaa vinavyotumika kwenye ujenzi vinapimwa kwenye maabara za ujenzi na taratibu za manunuzi zinafuatwa ili kuhakikisha miradi inayotekelezwa inakuwa na ubora uliokusudiwa.

**ELIMU KWA UMMA**

TAKUKURU mkoa wa Mbeya katika kipindi cha mwezi Aprili hadi Juni 2020 iliendelea na jukumu la kuelimisha umma kwa kuwataka wananchi kutojiingiza katika vitendo vya rushwa, ambapo tuliweza kuelimisha zaidi ya wananchi wapatao 1570 kwa njia ya semina ,klabu za wapinga rushwa, mikutano ya hadhara na vipindi vya radio.

**UCHUNGUZI NA MASHTAKA**

Katika kipindi cha Aprili hadi Juni tulipokea jumla ya taarifa 136 za tuhuma za rushwa na makosa mengine kwa mchanganuo ufuatao: Halmashauri taarifa 29, Sekta binafsi (wafanyabiashara) taarifa 19, Mashirika ya Umma taarifa 11, Vyama vya ushirika taarifa 9, mahakama 12, , Polisi taarifa 12, idara ya ardhi taarifa 12, Maliasili taarifa 1, elimu taarifa 4, uhamiaji taarifa 1, madini taarifa 3, uchaguzi taarifa 6 , vyama vya wafanyakazi taarifa 1, sekta ya afya taarifa 3 na mifuko ya hifadhi ya jamii taarifa 3.

Katika kipindi hicho TAKUKURU mkoa wa Mbeya iliendesha na kesi 16 mahakamani, na kuweza kufungua kesi 5, kushinda kesi 4 na kushindwa kesi 1.

**MWELEKEO WETU**

Ninafahamu kuwa sote tunajuwa kuwa nchi yetu inaelekea kwenye uchaguzi mkuu mwezi Octoba 2020, hivyo TAKUKURU Mkoa wa Mbeya katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai hadi Septemba 2020 tumejipanga kufanya mambo yafuatayo: -

kuendelea kuelimisha wananchi juu ya rushwa na madhara yake katika uchaguzi lengo ni kuwawezesha wananchi kupata uelewa na kuweza kuchaguwa viongozi waadilifu na wazalendo, wachapa kazi watakaowaletea wananchi maendeleo na wasiojihusisha na vitendo vya rushwa.

Tutaendelea kufanya kazi za utafiti na udhibiti kwa lengo la kubaini mianya ya rushwa katika maeneo mbalimbali ya uchaguzi, taasisi za Umma na Binafsi na kushauri namna bora ya kuiziba mianya hiyo.

Tutaendelea kufanya uchunguzi na kuwachukulia hatua wale wote watakao kutwa na tuhuma za vitendo vya rushwa ikiwa ni pamoja na kuwafikisha Mahakamani.

Pia tutaendelea kukagua na kufuatilia miradi mbalimbali ya maendeleo inayoendelea kutekelezwa na ile itakayokuwa inaanza kutekelezwa ndani ya Mkoa pamoja na kuendelea kufuatilia madeni sugu yanayohusu AMCOS na SACCOS katika mkoa wa Mbeya.

Baada ya kusema hayo nipende kuwapongeza wananchi wote wa mkoa wa Mbeya kwa jinsi wanavyoendelea kushirikiana na TAKUKURU kufichua vitendo vya rushwa. Ninawasihi kuendelea kushirikiana na TAKUKURU katika mapambano dhidi ya rushwa, kutokubali kutoa au kupokea rushwa, kutoa taarifa za vitendo vya rushwa na kutoa ushahidi pale watakapohitajika.

**JULIETH MATECHI**
**MKUU WA TAKUKURU MKOA WA MBEYA**
***JULAI, 2020***